Kupalia Mkaa Wa Moto Katika Kichwa Cha Adui Yako

(Burning Coals On Your Enemy's Head)

Na

Ellis P. Forsman

Kupalia Mkaa Wa Moto Katika Kichwa Cha Adui Yako

(Burning Coals On Your Enemy's Head)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 11, 2011

Kupalia Mkaa Wa Moto Katika Kichwa Cha Adui Yako

Rum. 12:17-21

Ni vigumu sana – kusema kidogo – kumkirimia mtu anayekutendea maovu. Mtu huyu ni adui yako – mtu ambaye yuko kinyume na wewe.

Maadui hawa wanaweza kuwa majirani zako, wafanya kazi wenza, ikiwezekana hata marafiki. Utawajibuje watu ambao ni maadui zako?

Kama hujui, basi somo hili litakusaidia kuona ulinganifu kati ya mwili na roho zinavyofanya kazi.

Kama hufahamu, somo hili litakusaidia kustawisha matakwa yako katika kutenda mapenzi ya Bwana.

Jinsi ambavyo mwili unafanya kazi

Ukitendewa mabaya, ni *halisia* kutafuta kulipa kisasi. Wengine huthibitisha "mabega baridi" ili kutokuwa na hatia ya "kisasi".

Hata kama hakuna kitu kilichofanywa au kusemwa, roho inaweza kulaumiwa kwa kutokuwa na nia sahihi dhidi ya adui yako.

Kuchukua sheria mkononi katika hatua binafsi. Mat. 5:38, "*Mmesikia kwamba imenenwa, jicho kwa jicho na jino kwa jino;*"

Sheria ya Musa iliruhusu adhabu kuwepo kwa ajili ya uhalifu.

- Kumb. 19:21, "*Wala jicho lako lisiwe na huruma; uzima kwa uzima, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu.*"
- Law. 24:20, "*Jeraha kwa jeraha, jicho kwa jicho, jino kwa jino; vile vile kama alivyomtia mtu kilema, naye atalipwa vivyo.*"

Sheria ya Musa haikuruhusu mtu kulipiza kisasi kwa mkono wake mwenyewe.

Wakati hakuna udhuru mbele za Mungu kwa tabia kama hiyo, Wakristo wengi wamekuwa na hatia ya kwenda kinyume na mapenzi ya Mungu katika hali kama hii. Rum. 7:14-15, "*Kwa maana twajua ya kuwa torati asili yake ni ya rohoni; bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi. Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda.*"

Baadhi ya wakristo wengine hawafikirii mara mbili kuhusu kufanya kile ambacho wangelichukia. Wakristo wengine wanaweza "kufikiria mara mbili" alafu bado wanaendelea kulipa ovu kwa ovu.

Haijalishi jinsi mtu anavyojaribu kujithibitisha mwenyewe, neno la Mungu linakataa kulipa ovu kwa ovu. Rum. 12:17, "*Msimlipe mtu ovu kwa ovu. Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote.*"

Barikini wale wanawatesa

Yesu anawataka wafuasi wake kuwapenda maadui zao. Dunia inawapenda majirani zao na kuwachukia maadui zao.

Mkristo anaomba na kumtendea adui yake mema.

- Mat. 5:44, "*Lakini mimi nawaambia wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi,*"
- Luka 6:27, "*Lakini naambia ninyi mnaosikia, wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi,*"

Hiki ndicho ambacho Bwana wetu alionyesha katika ulimwengu. Luka 23:34, "*Yesu akasema Baba uwasamehe kwa kuwa hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake wakipiga kura.*"

Alafu, kuwapenda maadui zetu inakwenda kinyume na uhalisia wa asili yetu. Mat. 5:43, "*Mmesikia kwamba imenenwa, umpende jirani yako, na umchukie adui yako.*"

Ni vigumu kumwombea kiongozi au serikali amabo wanakandamiza maisha yako. 1 Tim. 2:2, "*Kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu.*"

Ni vigumu "kutenda mema" kwa maadui waliokufanya mtumwa wao. 2 Fal. 5:1-4, "*Basi Naamani, jemadari wa jeshi la mfalme wa Shamu, alikuwa mtu mkubwa mbele ya bwana wake, na mwenye kuheshimiwa, kwa sababu kwa mkono wake BWANA alikuwa amewapa Washami kushinda; tena alikuwa mtu hodari wa vita; lakini alikuwa mwenye ukoma. Na Washami walikuwa wametoka vikosi, wakachukua mfungwa mmoja kijana mwanamke kutoka nchi ya Israeli; naye akamhudumia mkewe Naamani. Akamwambia bibi yake, laiti bwana wangu angekuwa pamoja na yule nabii aliyeko Samaria! Maana angemponya ukoma wake. Mtu mmoja akaingia, akamwambia bwana wake akasema, yule kijana mwanamke aliyetoka nchi ya Israeli asema hivi na hivi.*"

Alafu, wale wanaojitaahidi kuwa kama Baba yetu wa mbinguni watajitahidi kufanya hili. Mat. 5:48, "*Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.*"

Kumpalia adui yako mkaa

Kumfanyia adui yako memo huzalisha mrundikano "kuchoma mkaa katika kichwa chake". Rum. 12:17-21, "*Msimlipe mtu ovu kwa ovu. Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote. Kama yamkini kwa upande wenu, make katika amani na watu wote. Wapenzi msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa kisasi ni juu yangu mimi, mimi nitalipa anena Bwana. Lakini adui yako akiwa na njaa, mlishe; akiwa na kiu mnyweshe; maana ufanyapo hivyo utampalia makaa ya moto kichwani pake. Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema.*"

Kinyume na jinsi wengine wanavyofikiri, huu siyo upotovu fulani "njia ya kimungu" ya kupata kisasi. Kufuata mapenzi ya Bwana kunakufaidisha wewe na adui yako. Kwa lugha nyingine, mtendee adui yaako kama rafiki yako.

Huu ndiyo aina ya upendo ambao Mungu ameonyesha kwetu. Rum. 5:6-10, "*Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki kwa damu yake tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye. Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tukaokolewa katika uzima wake.*"

Hii ndiyo aina ya upendo wa dhati mtu Paulo anayowasii ndugu kule Rumi ili watende. Rum. 12:9, "*Pendo lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema.*"

Hitimisho

Ni vigumu kumtendea mema adui yako kwa upendo. Vile vile, hiki ndiyo humtenganisha Mkristo wa kweli na ufalme wa milele wa Mungu.